# OFISI YA RAISI
# TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MTAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

Shuleya sekondari Muyenzi,

S.L. P. 05,

RULENGE – NGARA.

09/06/2017.

**Simu : 0622767611/0768906072/0628200716/0743898853**
**Kumbu.Na.ED/MSS/SF/14/2017.**

**MWANAFUNZI…………………………………………………………………….**
**S.L.P……………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………….**

**YAH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MUYENZI 2017**

1.0 Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidatao cha tano katika shule hii mwaka 2017. Kwa mchepuo wa**HGL/HGK**.

Shule ya **Sekondari Muyenzi** ipo wilaya ya **Ngara**, mkoa wa **Kagera**,umbali wa kilometa 52 kusini magharibi ya makao makuu ya wilaya.Usafiri kutoka Ngara mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Ngara, ukishukakatika kituo hiki uliza magari yanayoelekea Bugarama, shuka Muyenzi sekondari,nauli ni shilingi 5,000/=. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 03/07/2017. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 17/07/2017.

2.0 **Mambo Muhimu ya Kuziangatia.**

2.1 **Sare ya shule**.

Unatakiwa kuleta sketi mbili za rangi ya “Dark Blue” (cotton).Mshono wa sketi ni “Rinda box” (V) urefu nchi 3 chini ya goti.

- **i.** Shati mbili nyeupe za mikono mirefu aina ya tetroni,iliyo na alama ya kirumi ya kidato cha tano mabegani, ya kitambaa cha rangi ya Dark Blue. Nembo ya shule inapatikana hapa shuleni
- **ii.** Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili vya kamba na vyenye kisigino kifupi.**Usije na viatu visivyo vya kamba.**
- **iii.** Tai yenye rangi ya kitambaa cha sketi.
- **iv.** Soski jozi 02 nyeupe ndefu.
- **v.** Sweta 02 kwaajili ya baridi(Rangi za Bendera ya Taifa)
- **vi.** T-Shirt 02 za kushindia baada ya masomo rangi ya blue na yenye kola kitambaa cha cotton, sketi 02 za rangi ya kijani pamoja na gauni 01 ya light blue,(yenye marinda12-15 na mikanda ya kufungia nyuma), sketi ya kushindia ni kitambaa cha sukari na gauni ni kitambaa cha sukari pia.

*Hijabukwa wasichana wakiislamu watakaopenda kuvaa hivyo. Rangi ya hijab ifanane na sareya shule iliyotajwa hapo juu.

**2.2Ada na michango ya shule**

**a) Ada ya Shule**

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=. Unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa muhula mmoja au zote shilingi 70,000/= kwa mara moja. Fedha hii iwekwe kwenye akaunti ya shule ya **NMB**, **Muyenzi Secondary School Capitation Grant A/C. No. 32101200060**,katika tawi lolote la NMB. Mwanafunzi ajapo shuleni aje na "**Bank Pay Slip".** Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip. Mwanafunzi ambaye hatakuja na Bank Pay Slip hatapokelewa.

**a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

i. Tsh. 6000/=kwaajili ya kitambulisho na picha.
ii. Tsh 15,000/=kwaajili ya ukarabati na samani.
iii. Tsh 30,000/=kwaajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
iv. Tsh 2,000/=kwaajili ya nembo.
v. Tsh 10,000/=kwa ajili ya huduma ya kwanza na bima ya afya. kama una bima njoo nayo (kija na bima hakuzuii kulipa shililngi 10,000/=)
vi. Tsh 5,000/=Tahadhari (haitarejeshwa)
vii. Tsh 20,000/= kwa ajili yaTaaluma
viii. Tsh 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima *mock*

Kwa wale wanaolipiwa na wafadhili wakumbuke kuleta uthibitisho wa maandishi yanayoonesha aina ya malipo watakayolipiwa na yatalipwa lini.

**2.3 Vifaa vya malazi,chakula na usafi.**

i. Unatakiwa kuwa na jembe mojalenye mpini,pamoja na siko/kotama moja kwaajili ya kufanyia usafi .
ii. mifagio 02 ya rangi ya blue, mmoja kwa ajili ya kufagia nje, na mwingine kwa ajili ya kufagia ndani
iii. Godoro la 21/2 X 6.
iv. Sahani ,kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula.
v. Ndoo 02ndogo zaplastic zenye mifuniko.
vi. Chandarua moja rangi nyeupe .
vii. Blanket moja
viii. Mashuka pair mbili za rangi ya pinki.
ix. foronya moja

**2.4 Vifaa vya masomo**.

i. Daftari 7 kubwa kwa kuanzia (Counter Book QUIRE 3).
ii. Daftari 10 ndogo kwaajili ya majaribio ya mwezi.
iii. Kalamu ya wino- bluu au nyeusi
iv. Mfuko wa vitabu (School bag)
v. Ream moja (1) ya karatasi za photocopy (A4).
vi. Vitabu vya masomo utakayo yasoma.

2.5 **Vifaa vya Michezo**.

Unatakiwa kuwa na vifaa vya michezo vifuatavyo, ili kuvitumia wakati wa michezo mbalimbali hapa shuleni na nje ya shule.

i. Viatu vya raba (vyeusi).
ii. Jezi za rangi ya bluu (tracksuit).

2.6 **Vifaa vingine**

Unatakiwa kuja na vifaa vya matumizi ya kila siku kama vile; taulo,dawa ya meno, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta n.k. Ni vyema pia ukaja na sanduku la mbao au la bati kwaajili ya kutunzia vifaa vyako. Kumbuka nguo za kiraia ambazo si uniform za shule na ambazo hazikutajwa katika fomu hii haziruhusiwi kuvaliwa shuleni.***Mwanafunzi haruhusiwa kuja navipodozi hasa vya kujiremba na kuchubua ngozi.***

3.0 **Mahitaji mengine**.

a) Unatakiwa kuleta picha nne(4) ndogo (passport size) za rangi kwaajili ya kitambulisho na matumizi mengine ya kiofisi.
b) Unatakiwa kuleta cheti cha uraia.
c) Afya ya mwanafunzi
   Nimeambatisha “Medical Examination Form” ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwamkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.

Muhimu; hakikisha inajazwa kwa usahihi kuepuka usumbufu utakaojitokeza kwani hatutapokea maelezo yam domo kuhusiana na afya ya mwanafunzi isipokuwa akiugua shuleni.

d)Naaambatisha fomu ya kuandikishwa shuleni,pamoja na ahadi ya Mzazi/Mlezi.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA.**
**SHULE YA SEKONDARI – MUYENZI**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Pamoja na fomu hiiya kujiunga na shule naambatisha sheria za shule hii.

Sheria na kanuni za shule zinatungwa kufuatana na maadili ya Taifa letu.Lengo ni kutoa mwongozo na msaada kwamwanafunzi ambaye anatarajiwa awe raia na Mzalendo wa Jamuhuri yaMuungano wa Tanzania. Utii wa sheria za shule ni utii wa sheria za taifa letu. Shule imepewa jukumu la kulea na kuelimisha vijana ili baadae wawe raia wema wa Taifa hili. Sharti mwanafunzi kufuata kanuni na sheria za shule. Zifuatazo ni sheria za shule nakila mwanafunzi anatakiwa aziheshimu na kuzizingatia ipasavyo:-

1. Mwanfunzi sharti awaheshimu walimu na wafanyakazi wote wa shule ambao ni walezi wake. Ajiepushe na lugha chafu, utovu wa nidhamu kwa walezi hawa. Inampasa mwanafunzi kusimama sawa anapomwona mwalimu au mfanyakazi na mgeni yeyote ambaye anamzidi umri na kumwamkia ipasavyo.
2. Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kukataa kufanya kazi za shule,au adhabu ya mwalimu au kiongozi yeyote Yule wa wanafunzi aliyechaguliwa kwa mujibu wa sheria.
3. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na nje alivyopangiwa kwa wakati uliopangwa. Ni kosa kubwa kukosa vipindi bila sababu maalum.
4. Ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule isipokuwa kwa kibali maalum cha Mkuu wa shule,kila mwanafunzi atawajibika kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezojuu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
5. Kila mwanafunzi atalazimika kuzingatia ratiba ya siku nzima na kuitekeleza “Daily Routine”
6. Kila mwanafunzi analazimika kuvaa sare ya shule wakati wote.
7. Kila mwanafunzi atalazimika kuhudhuria maandalio ya jioni (Preparation).
8. Ni lazima mwanafunzi ajiepushe na makosa ambayo yanaweza kusababisha afukuzwe shule.Makosahayo ni haya yafuatayo;
    i. Wizi
    ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
    iii. Uasherati, Ubakaji, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
    iv. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
    v. Uvutaji wa sigara
    vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.

vii. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule

viii. Kufuga ndevu

ix. Kuharibu kwa makusudi maliya umma

x. Kudharau Bendera ya Taifa na picha za viongozi wakuu wa Serikali

xi. Kupata mimba au Kutoa au kushiriki kutoa mimba

xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana ndani na nje ya shule

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi(Makosa ya jinai)

xiv. Kugoma, kuhamasisha mgomo, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu

xv.Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla

xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

xvii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule).

xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

9.Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:-

- Chumba cha walimu
- Ofisi za shule
- Maabara
- Jikoni
- Nyumba za Walimu na Wafanyakazi wasio Walimu

**SHULE YA SEKONDARI MUYENZI**
**FOMU YA KUANDIKISHWA-SHULE**

(Ijazwe kwa herufikubwa na irejeshwe kwa mkuu wa shule)

1. Jina kamili………………………………………………………………………………………………………
   Tarehe ya kuzaliwa……………………Wilaya……………………Mkoa………………………
   Taifa………………………………………Dini:RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecoste/n.k…………………..
   Shuleya sekondari uanayotoka……………………………………………………………………………………………..
2. Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi……………………………………………………………………………………………..
   Anwani yake ………………………………………………………………………………………………………..
   Kazi ya Baba/Mama/Mlezi……………………………………………………………………………………..
   Namba ya simu…………………………………………………………………………………………………………………..

AHADI YA MWANAFUNZI.

a) Mimi……………………………………………………………………nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha TANO katika shule ya sekondari Muyenzi kuanzia tarehe……………………hadi nitakapomaliza kidato cha SITA.
b) Kwahiyo naahidi kwamba:-
   i. Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa
   ii. Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa shule na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.Kama kushiriki migomo, fujo,makosa ya jinai n.k
   iii. Nitatunza mali za umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabun.k

Tarehe……………………………………………………Sahihi ya Mwanafunzi………………………………………………..

AHADI YA MZAZI/MLEZI.

Mimi:……………………………………………………………………ambaye ni Mzazi /Mlezi wa
Mwanafunzi…………………………………………………………………………………………………………..
Ninaahidi kwamba :-

1.Nitashirikiana na uongozi wa Shule,Walimu na Watumishi wasio walimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za Shule ya Sekondari Muyenzi. Iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongozi wa shule.

2.Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kusoma kwa kulipa ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa na shule.

Sahihi…………………………………………………
Tarehe…………………………………………………..
Namba ya simu…………………………………………………………………………………………………….

***Kumbuka kuleta picha kuleta picha nne (04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.**

NGARA DISTRICT COUNCIL
MUYENZI SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(Ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali)

To be completed by medical Officer in respect of Muyenzi Secondary School Student(Entrant).

1. Full name of student…………………………………………………………………………………………………..
2. Sex……………………………………………Age…………………………………………………….
3. HGB Test…………………………………………………………………………………………………………
4. Stool……………………………………………………………………………………………………..
5. Urine
   Micro………………………………………………………………………………………………………….
6. T.B
   Test…………………………………………………………………………………………………………….
7. Eye Examination………………………………………………………………………………………
8. E.N.T……………………………………………………………………………………………………………
9. Chest…………………………………………………………………………………………………………..
10. Abdomen…………………………………………………………………………………………………………..

ADDITIONAL INFORMATION.

Physical Defects or Impairment, Infections, Chronic or Hereditary(family) diseases.

………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above student and consider that* he/she is physically/not physically fit for further studies.

NAME…………………………………………………………………………..
SIGNATURE…………………………………………………………………

DATE……………………………………………………………………………
OFFICIAL STAMP

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

Uongozi wa shule unakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa shuleni.

Saini ya Mkuu wa Shule………………………………

Jina La Mkuu wa Shule…………………………..……

Mhuri wa Mkuu wa Shule………………………………

**ORODHA YA BAADHI YA VITABU VYA MASOMO**

JIOGRAFIA

1. Msabila , D. T.(2014) (A Comprehensive Approach To Physical Geography
2. Kamili, Z(Current Edition) Practical Geography Alive

HISTORIA

1. Kato A.K ( 2014)
   Mastermy History
2. Zisti Kamili – Advanced History Part One Alive
3. Herbert L. Peacock(1982). A History of Europe .London ltd Britan or Tumain
4. C.K Shibital (2013).Contemporay Historical , Events
5. Bruun G & Ferguson K.W (1958) A Survey of European Civilization ,Part one Boston

KISWAHILI

1. Nadharia Ya Kiswahili 1- Kidato Cha Tano na Sita

2. Nadharia Ya Kishwahili 2- Kidato Cha Tano na Sita

KIINGEREZA

1. Recommended English Language One Text Book For A- Level Student
   ( By Paschal Salawi)
2. Advanced Level Literature By Nyambari Nyangwine And Godfrey Rutta Bukagile
3. English Language One For Advanced Level New Syllabus By Michael Kadeghe.
4. English Language One By Mcholaus Ashel
5. Dictionary English To English
6. Novel- His Excellence Head Of State
   - A Man Of The People
   - An Enemy Of The People
   - The Beautiful Ones Are Not Yet Born